Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

# Wanyama wa Misitu ya Rubeho

**Milima ya Rubeho** iliyopo katika Wilaya za Mpwapwa na Kilosa ni sehemu ya Milima ya Tao la Mashariki. Misitu ya Milima ya Rubeho ni muhimu sana kwa sababu inalinda vyanzo vya maji na udongo na hutoa mimea itumikayo kama dawa. Misitu hii pia ni muhimu kwa sababu inategemewa na aina nyingi za mimea na wanyama. Baadhi ya hii mimea na wanyama haipatikani mahali pengine duniani.

Kuna zaidi ya aina 132 za ndege, aina 40 za mamalia (wanyama wanyonyeshao), aina 14 za wanyama jamii ya nyoka na mijusi na aina 14 za wanyama jamii ya vyura ambao wanaishi katika Misitu ya Rubeho. Aina nyingi za wanyama hawa wanaishi tu msituni na watakufa endapo misitu hii ikiharibiwa.
Baadhi ya misitu muhimu katika Milima ya Rubeho ni pamoja na Mafwemela, Ipondelo, Mang'alisa, Ukwiva na Ilole. Misitu hii ipo katika hatari ya kuathiriwa na ukataji wa miti kiholela, mioto na ufyekaji kwa ajili ya kilimo.



**Kwale wa Rubeho**
Jina la Kisayansi: *Xenoperdix obscurata*
Kwale huyu wa Rubeho anapatikana katika misitu ya Mafwemela na Ipondelo pekee. Kwale huyu anategemea misitu kwa kuishi.

*Picha na Jon Fjeldså*

Kuna aina nane za vyura ambao wanapatikana katika Misitu ya Rubeho pekee na si pengine duniani.



**Jina la kisayansi:** *Nectophrynoides* Sp. Nov.
Aina hii ya chura wa msituni ni aina mpya katika sayansi. Chura huyu anapatikana katika Milima ya Rubeho pekee.



**Jina la kisayansi:** *Probreviceps* Sp. Nov.
Aina mpya ya chura mwenye vidole vikubwa. Chura huyu aligunduliwa katika msitu wa Ilole na Mafwemela na timu ya watafiti wa bioanuwai kutoka TFCG pamoja na Trento. Chura huyu anapatikana katika misitu ya Rubeho pekee.



**Jina la kisayansi:** *Leptopelis* Sp. Nov.
Aina hii ya chura aishiye kwenye miti ni aina mpya katika sayansi. Anapatikana katika Misitu ya Rubeho pekee.



**Chura wa Nike**
Jina la kisayansi: *Arthroleptis nikeae*
Chura huyu anapatikana katika misitu ya Mafwemela na Ipondelo pekee.



**Kinyonga mwenye pembe tatu**
Jina la kisayansi: *Chamaeleo werneri*
Kinyonga huyu anapatikana katika Milima ya Tao la Mashariki pekee.



**Kinyonga Mdogo**
Jina la kisayansi: *Rhampholeon moyeri*
Kinyonga huyu anapatikana katika Milima ya Tao la Mashariki pekee.



**Nyoka wa Tornier**
Jina la kisayansi: *Crotaphopeltis tornieri*
Aina hii ya nyoka wa msituni anapatikana katika sehemu chache za misitu ya mlimani ya Tanzania na Malawi tu.



**Jina la kisayansi:** *Scolecomorphus kirkii*
Huyu mnyama anafanana nyoka lakini anatabia ya vyura zaidi.



**Nungunungu**
Mnyama huyu ana tabia ya kutembea hasa nyakati za usiku. Anakula mizizi, magome ya miti na matunda ya miti yaangukayo. Ingawa wako maeneo mengi ya Kaskazini mwa Afrika ni nadra sana kuonekana



**Minde**
Funo huyu mkubwa anapatikana katika sehemu chache za misitu ya mlimani hapa Tanzania ikiwemo misitu ya Rubeho.



**Kanu wa Lowe**
Huyu ni mnyama mla nyama ambaye hupatikana katika Milima ya Tao la Mashariki na Zanzibar pekee.



**Komba wa Mlimani**
Komba huyu mdogo wa milimani ni mnyama jamii ya primata ambaye hutembea wakati wa usiku. Komba hawa huishi kwa kutegemea misitu.

## TUSHIRIKIANE KATIKA KUILINDA MISITU YA MILIMA YA RUBEHO

Taarifa katika bango hili imetokana na tafiti za bioanuwai zilizofanywa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) pamoja na Taasisi ya Makumbusho ya Historia ya Asili ya Trento 2006.

*Mpiga Picha: Michele Menegon na Francesco Rovero*

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

MUSEO TRIDENTINO DI SCIENZE NATURALI

# Wanyama wa Misitu ya Mufindi

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Misitu ya Milima ya Udzungwa iliyoko katika Wilaya ya Mufindi ni sehemu ya Milima ya Tao la Mashariki. Misitu hii ni muhimu sana kwa sababu inalinda vyanzo vya maji na udongo na ina mimea itumikayo kama dawa. Misitu hii pia ni muhimu kwa sababu inategemewa na aina nyingi za mimea na wanyama. Baadhi ya hii mimea na wanyama haipatikani mahali pengine duniani.

Kuna zaidi ya aina 126 za ndege, aina 37 za mamalia (wanyama wanyonyeshao), aina 27 za wanyama jamii ya nyoka na mijusi na aina 20 za wanyama jamii ya vyura ambao wanaishi katika Misitu ya Mufindi. Aina nyingi za wanyama hawa wanaishi tu misituni na watatoweka endapo misitu hii ikiharibiwa.

Kuna aina 10 za wanyama wenye uti wa mgongo wanaopatikana Mufindi ambao hupatikana katika milima ya Udzungwa pekee duniani. Aina hizi ni pamoja na aina nne za vyura, aina moja ya kirukanjia, aina mbili za nyoka, aina moja ya mjusi na aina mbili za vinyonga.

**Athari katika misitu hii**

Misitu hii inatishio na imeathiriwa na mioto, ufyekaji wa misitu kwa shughuli za kilimo, mbao na nguzo.

Taarifa katika bango hili imetokana na tafiti za bioanuwai zilizofanywa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) pamoja na Taasisi ya Makumbusho ya Historia ya Asili ya Trento, Italia mwaka 2006.

*Mpiga Picha: Michele Menegon na Francesco Rovero*



**Chura aishiye kwenye migomba**
Jina la kisayansi: *Afrixalus* Sp. Nov.
Aina hii ya chura wa msituni ni aina mpya katika sayansi. Chura huyu anapatikana katika Milima ya Udzungwa pekee.



**Chura aishiye kwenye miti**
Jina la kisayansi: *Leptopelis* Sp. Nov.
Aina hii ya chura aishiye kwenye miti ni mpya katika sayansi. Anapatikana katika Misitu ya Mufindi pekee.



**Chura mwenye vidole vikubwa**
Jina la kisayansi: *Probreviceps* Sp. Nov.
Aina hii ya chura wa msituni ni aina mpya katika sayansi. Chura huyu aligunduliwa katika msitu wa Kigogo na timu ya watafiti wa bioanuwai kutoka TFCG pamoja na Trento. Chura huyu anapatikana katika misitu ya Mufindi pekee.



Jina la kisayansi: *Phlyctymantis keithae*
Chura huyu anapatikana katika Milima ya Udzungwa pekee.




**Kinyonga wa msituni**
Jina la kisayansi: *Kinyongia* Sp. Nov.
Aina hii ya Kinyonga ni aina mpya katika sayansi. Kinyonga huyu aligunduliwa katika msitu wa Kigogo na timu ya watafiti kutoka TFCG pamoja na Trento. Kinyonga huyu anapatikana katika Milima ya Udzungwa pekee.



**Kinyonga wa ndevu mbili**
Jina la kisayansi: *Chamaeleo tempeli*
Kinyonga huyu anapatikana katika Milima ya Udzungwa na Kipengere pekee.



**Nyoka aina ya moma** akila aina mpya ya chura ambae huishi kwenye migomba.



**Nyoka mwenye pua nyekundu wa Udzungwa**
Jina la kisayansi: *Lycophidion uzungwense*
Aina hii ya nyoka anapatikana katika Milima ya Udzungwa pekee.



**Komba wa Milimani**
Komba wadogo wa Mufindi wameonekana kutofautiana na komba wengineo wadogo wanaopatikana kwenye milima mengine. Utafiti wa kubaini utofauti huu bado unaendelea kufanyika. Komba wa milimani huishi kwa kutegemea misitu.



**Jina la Kiingereza: African Palm civet**
Mnyama huyu mwenye tabia ya kujificha anategemea sana misitu kuishi.



**Kanu ya Lowe**
Huyu ni mnyama mla nyama hupatikana katika Milima ya Tao la Mashariki na Zanzibar pekee.



**Kinyonga mwenye miiba mgongoni**
Jina la kisayansi: *Chamaeleo laterispinis*
Aina hii ya Kinyonga anapatikana katika Milima ya Udzungwa pekee .

**Tumepoteza nini?**
Si kipindi kirefu sana hapo nyuma ambapo chui, nyati, funo, perere na hata tembo walikuwa wanapatikana katika misitu ya Mufindi. Wanyama hawa wameadimika sana na huenda wameshatoweka kabisa katika misitu hii.

**TUSHIRIKIANE KATIKA KUILINDA MISITU YA MUFINDI**

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

MUSEO TRIDENTINO DI SCIENZE NATURALI